

Chanjo za COVID-19 za Pfizer/BioNTech na Moderna: Je, Zinatofautiana?


Tarehe 7 Juni, 2021

Kimsingi, chanjo za COVID-19 za Pfizer/BioNTech na Moderna zinafanana – zote mbili ni fanisi zaidi, ni salama zaidi na zimefanyiwa utafiti wa kutosha.



Kimsingi, chanjo za Moderna na Pfizer/BioNTech ni bidhaa moja iliyotengenezwa na makampuni tofauti.

Zinalinganishwa na chapa mbili za maji ya chupa – bidhaa moja lakini imetayarishwa na makampuni tofauti.



Chanjo hizi zinafanya kazi kwa njia sawa – zote mbili ni chanjo za mRNA.

Zote mbili zinatoa maagizo (“mRNA”) ya kufunza mfumo wa kinga ya mwili wako kutambua virusi vya COVID ili uweze kupambana na kushinda maambukizi haya ikiwa utaambukizwa virusi halisi vya COVID-19 baadaye. Chanjo hizi hazina virusi.



Chanjo zote mbili ni fanisi zaidi katika kutoa ulinzi dhidi ya ugonjwa wa COVID.

Katika tafiti kubwa za kisayansi zilizofanywa, chanjo zote mbili zilipatikana kuwa na ufanisi wa asilimia 95 katika kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa COVID baada ya mtu kupokea dozi mbili.

Tafiti zinaonyesha kuwa chanjo zote mbili ni fanisi zaidi katika kuzuia vifo au magonjwa ya kulazwa hospitalini yanayohusiana na COVID, katika tukio lisilo la kawaida ambapo mtu aliyepokea chanjo ataambukizwa.



Chanjo zote mbili zina madhara ya kiafya yanayofanana, ambayo si makali na yanayodumu kwa muda mfupi.

Madhara ya kiafya yanayoweza kutokea sana ni pamoja na kuhisi uchungu kwenye bega/mkono mahali ambapo ulidungwa sindano, kuhisi uchungu mwilini na kwenye misuli, kuhisi baridi, kuhisi uchovu na kuwa na dalili za kuongezeka kwa joto mwilini. Kwa kawaida madhara haya ya kiafya hupungua baada ya karibu siku moja hadi tatu.

Chanjo zote mbili hazina madhara mabaya kwa ujauzito au kwa uwezo wako wa kupata watoto. Chanjo zote mbili hazisababishi kuganda kwa damu.

Chanjo zote mbili hudungwa karibu na bega – kwa haraka sana na bila kuhisi uchungu mwingi. Uchungu unaohisi kutokana na kudungwa chanjo zote mbili ni sawa.



Kliniki na maeneo ya kutoa chanjo hupokea mojawapo ya chanjo hizi, kulingana na chanjo inayopatikana.

Usafirishaji wa kila mojawapo ya chanjo hizi nchini Kanada unaweza kutofautiana kila wiki.



Chanjo za Pfizer/BioNTech na Moderna zina ufanisi sawa. Pokea mojawapo ya chanjo hizi unayopewa, kwa kufahamu kuwa zote mbili zitakulinda wewe na uwapendao dhidi ya kuambukizwa ugonjwa wa COVID-19.



Tunatumai taarifa hii itakufaa! Tunakuomba usambaze taarifa hii kwa wingi, uitumie kama hati ya kurekodi faili ya sauti au video au kuitafsiri katika lugha nyingi ili uisambaze kwa wengine. Tafadhali hakikisha umetaja chanzo: Women's College Hospital, OCASI, TAIBU Community Health Centre and Refugee 613.

Taarifa hii ni sahihi kufikia tarehe 7 Juni, 2021

Maelezo yaliyo katika taarifa hii yamethibitishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu cha Toronto; Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Toronto; na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo Kikuu cha Toronto

{ REFUGEE } 613

BE IN GOOD HEALTH
TAIBU
COMMUNITY
HEALTH CENTRE

OCASI
Ontario Council of Agencies Serving Immigrants

WCHI
WOMEN'S COLLEGE HOSPITAL
Healthcare | REVOLUTIONIZED

Funded by:



Immigration, Refugees
and Citizenship Canada

Financé par :

Immigration, Réfugiés
et Citoyenneté Canada

With contributions from:

pchs 30
Serving Diverse Communities